

Maswali

1. Nani alikuwa mfalme baada ya Daudi?
2. Sulemani alikuwa na wasi wasi ya nini?
3. Sulemani aliota nini?
4. Sulemani angeuliza apewe nini yake mwenyewe?
5. Sulemani alichagua nini?
6. Mbona Sulemani alichagua hekima?
7. Mbona Mungu alifurahia chaguo la Sulemani?
8. Mungu alipea Sulemani nini pamoja na hekima?
9. Sulemani alikuwa mfalme wa namna gani?
10. Utawala wa Sulemani ulikuwa wa namna gani?

Majibu

1. Sulemani, mwana wa Daudi alikuwa mfalme baada ya Daudi.
2. Sulemani alikuwa kijana tu wakati alianza kuwa mfalme, alikuwa na wasi wasi vile angetawala watu wa Mungu.
3. Sulemani aliota kwamba Mungu alisema angechagua cho chote alichotaka na Mungu angempa.
4. Sulemani angechagua mali au nguvu au maisha marefu.
5. Sulemani alichagua hekima.
6. Alitaka awe mfalme mzuri tena mwenye busara.
7. Mungu alifurahi kwa sababu Sulemani hakujitakia cho chote chake ila alitaka asaidie watu wa Mungu.
8. Mungu alipea Sulemani mali, heshima na maisha marefu.
9. Sulemani alikuwa mfalme wa busara na mzuri.
10. Sulemani alikuwa na utawala mrefu wa amani.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



29 Sulemani

Marejeo

2 Mambo ya Nyakati 1: 7-13

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alimzawadisha Sulemani kwa kuchagua hekima imsaidie kutawala watu wa Mungu.

Maneno maalum

- 29.1 Sulemani + Mwana wa Daudi + mdogo + mfalme + ndoto + chagua cho chote + pesa + maisha marefu
- 29.2 Sulemani + watu + wasi wasi + omba hekima + taka kuwa mfalme mzuri
- 29.3 Mungu + furahi + Sulemani + si mchoyo + hekima + tawala vizuri + Mungu alipeana mali na heshima
- 29.4 Sulemani + busara + mfalme mzuri + utawala wa amani kwa muda

29.1 Sulemani alikuwa mwana wa Daudi. Alikuwa mfalme baada ya Daudi kukufa. Sulemani alikuwa mtoto sana alipokuwa mfalme. Alikuwa na wasi wasi sana sababu hakujuua vile atatawala watu wa Mungu na awafundishe kupenda na kumheshimu.

Usiku moja Sulemani aliota kwamba Mungu alikuwa amemwambia, “Chagua cho chote unachotaka na nitakupa?”

Mtu akikuuliza swali kama hilo, utataka nini? Labda ungetaka pesa ili uende ujinunulie kitu kizuri. Nina ukweli ungetaka kitu chenye ulikuwa ukitaka sana. Unafikiri Sulemani alichagua nini?



Kumbuka Mungu ndiye alimuuliza Sulemani alichotaka. Mungu alimuuliza cho chote, kwa hivyo angeuliza cho chote alichotaka. Unafikiri angeuliza amfanye awe na mali nyingi ili awe na pesa nyingi ya kutumia? Unafikiri angechagua kuwa na nguvu nyingi ili wafalme wengine wote wamwogope. Unafikiri angechagua kuwa na maisha mazuri na marefu.

29.2 Mfalme Sulemani hakuchagua moja ya hayo yote. Alifikiri juu ya watu wote wenye anaenda kutawala .

Watu wangemweendea wakati walikuwa na shida, na walitarajia yeye awasaidie. Wangukuja kwake kama wamegombana na awaamulie aliyekuwa na mkosa. Babake Daudi alikuwa mfalme mzuri, na Sulemani alitaka naye pia awe mfalme mzuri.

Sulemani alikumbuka mazuri yote yenye Mungu alimfanyia babake Daudi. Sulemani aliambia Mungu kwamba sasa yeye ni mfalme lakini alijisikia kama mtoto mdogo aliyepewa kazi kubwa sana ya kufanya. Sulemani aliuliza Mungu ampe hekima. Aliuliza Mungu amsaidie atawale Waisraeli na hekima. Aliuliza Mungu ampe hekima akiamua watu.

29.3 Mungu alifurahia Sulemani sana. Aliuliza jambo litakalo msaidia awe mfalme mzuri wa hekima ili awasaidie watu wake. Sulemani hakuwa na ubinafsi. Hakujitakia yeye mwenyewe.

Mungu alisema, “Nimefurahi kwa sababu umeuliza hekima ya kukusaidia utawale watu wangu vizuri. Haujuliza upewe maisha marefu, au uwe tajiri, au maadui wako wote wauawe. Nitakupa chenye umeuliza – moyo wa hekima na ufahamu. Lakini nitakupa pia na vitu vyenye haujuliza – mali na heshima. Kama utatii amri zangu na ufanye mambo yanayonipendeza, vile baba yako Daudi alifanya, nitakupea maisha marefu pia.”

29.4 Sulemani aliamka kutoka usingizini, alipata kwamba ni ndoto. Ilikuwa ndoto iliyokuwa ya kweli kwa sababu ilitoka kwa Mungu. Sulemani alikuwa mfalme wa hekima tena mzuri. Alikuwa na utawala wa muda mrefu tena wa amani.